# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA NNE

**31 AGOSTI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA NNE

## KIKAO CHA NNE – TAREHE 31 AGOSTI, 2026

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### WAZIRI WA FEDHA:

Maelezo ya Waziri wa Fedha kuhusu Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026.

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**37. MHESHIMIWA YUMNA MMANGA OMAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi wa kukuza vipaji na ujuzi kwa Vijana Wenye Ulemavu ili kuongeza ajira na ushiriki wao katika uchumi.

**38. MHESHIMIWA ASHA JUMA FERUZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali imewaunganishaje Wahitimu wa Kada zinazoendana na utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati nchini.

**39. MHESHIMIWA SAID ALI MBAROUK (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa utaratibu wa sasa wa Kikokotoo kwa Wastaafu wa Jeshi la Polisi ili kuboresha maslahi kwa Wastaafu.

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**40. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU (IKUNGI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Vituo vya Afya katika Kata za Minyughe, Igombwe, Muhintiri na Mwaru katika Jimbo la Ikungi Magharibi.

## WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

**41. MHESHIMIWA MDOWE HAJI KOMBO (NUNGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Vijana wanashirikishwa na kuwa sehemu ya upangaji Miji ya kisasa.

**42. MHESHIMIWA DICKSON NATHAN LUTEVELE (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kupima ardhi kwa bei nafuu kwa Wananchi wa Kata za Isalavanu, Bumilayinga, Rungemba na Saohill.

**WIZARA YA UJENZI:**

**43. MHESHIMIWA PATRICK ADKIN MWALUNENGE (MBEYA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya TANZAM kutoka Igawa hadi Mbeya Mjini kuunganisha Mbeya Mjini hadi Tunduma pamoja na *Bypass* utaanza.

**44. MHESHIMIWA BAZILIO KAPUNDA MBWILO (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Namanyere – Kipili Nkasi Kaskazini itajengwa kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**45. MHESHIMIWA FADHILI ALLY LIWAKA (NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini huduma za fedha kupitia mitandao ya simu zitapelekwa kwa Wananchi Kilimarondo na Kiegei ambao hufuata huduma hiyo umbali wa Km 120.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**46. MHESHIMIWA LUCY SIMIRYA KOMBANI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, hatua gani zinachukuliwa kuwalinda Watoto dhidi ya ukatili Mitandaoni kutokana na ongezeko la matumizi ya Mitandao ya Kijamii.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**47. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha somo la Historia ya Nchi yetu kuanzia Elimu ya Msingi ili kizazi kijacho kiwe na Uzalendo.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**48. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga jengo jipya la Mahakama ya Mwanzo Urambo kutokana na hali mbaya ya jengo lililopo sasa hasa kipindi cha mvua.

**WIZARA YA MAJI:**

**49. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, upi mpango wa kuwapatia maji ya Ziwa Victoria Wananchi wa Kata za Lyamidati Ilola, Puni, Nyida, Itwangi na Usanda – Shinyanga.

**WIZARA YA KILIMO:**

**50. MHESHIMIWA ALAN THOMAS MVANO (KAKONKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Mbegu za

Ruzuku kwa Wakulima wa Kakonko kwa Mazao ya Mahindi, Maharage na Mtama kwa msimu wa 2026.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**51. MHESHIMIWA MGORE MIRAJI KIGERA (MUSOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaiboresha Bandari ya Musoma Mjini ili ianze kufanya kazi na kufungua fursa za kiuchumi kwa Wananchi kupitia Ziwa Victoria.

## WIZARA YA MADINI:

**52. MHESHIMIWA AZIZA SLEYUM ALLY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, upi mchango wa Wachimbaji wakubwa na wadogo wa Madini kitakwimu ndani ya miaka Mitano.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**53. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itapitia upya Kanuni za Uvuvi ili kupunguza kero za tozo nyingi kwa Wavuvi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**54. MHESHIMIWA MOHAMED MUSSA UTALY (LINDI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendeleza Vivutio vya Utalii vilivyopo Lindi Mjini ili kuongeza mapato na ajira kwa Wananchi.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**55. MHESHIMIWA ATHUMIN OMARY MAPALILO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itaweka utaratibu maalum kwenye Viwanda vya Saruji Mkoani Mtwara ili kupunguza bei kwa kuwa uzalishaji unafanyika Mkoani humo.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026.

**DODOMA**
**31 AGOSTI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**